**HOSPITALI YA WATOTO YA DAYTON**
**SERA YA MSAADA WA KIFEDHA**

**SERA**:

Sera ya Msaada wa Kifedha ya Hospitali ya Watoto ya Dayton (DCH) inaafikiana na dhamira na maadili ya DCH na inaambatana na kujitolea kwa shirika hilo kwa jamii ambazo linazitumikia. Madhumuni ya sera hii ni kutambua taratibu wastani za kuamua msaada wa kifedha kwa wagonjwa wa DCH.

Huduma zinazoshughulikiwa na sera hii ni pamoja na Huduma zote za dharura na Huduma nyingine Muhimu za Kimatibabu zinazotolewa na Hospitali ya Watoto ya Dayton na Vituo Vingine Inavyomilika au Kushirikiana Navyo.

Hospitali ya Watoto ya Dayton itatoa, bila ubaguzi, huduma kwa hali za kimatibabu za dharura kwa watu bila kujali kama wanastahili msaada wa kifedha. DCH itatii Sheria ya Matibabu na Uzazi wa Dharura (EMTALA) kwa kutoa uchunguzi wa kimatibabu na kutoa matibabu ya kudhibiti hali, na kupeleka au kuhamisha mtu hadi kituo kingine inapofaa. DCH inakataza vitendo vyovyote vitakavyowawekea watu vikwazo wanapotafuta huduma za matibabu za dharura, kama vile kwa kudai kwamba wagonjwa katika idara ya dharura walipe kabla ya kupokea matibabu katika hali za matibabu ya dharura au kwa kuruhusu shughuli za kukusanya deni zinazoingilia utoaji, bila ubaguzi, wa huduma za matibabu za dharura.

**UFAFANUZI:**

**Kipindi cha Ombi** inamaanisha kipindi ambacho DCH lazima ikubali na kushughulikia ombi la usaidizi wa kifedha, lililowasilishwa na mtu binafsi, chini ya Sera yake ya Msaada wa Kifedha(FAP) ili kuweza kufanya juhudi mwafaka za kuamua ikiwa mtu huyo anastahiki kupokea msaada wa kifedha chini ya FAP. Kipindi cha Maombi huanza tarehe ambayo uangalizi hutolewa na kumalizika mwishoni mwa siku ya 240 baada ya tarehe ambayo taarifa ya kwanza ya bili baada ya kuondoka hospitalini ya huduma zilizolewa inatolewa au angalau siku 30 baada ya DCH kumpa mtu huyo taarifa ya maandishi ambayo inaweka tarehe ya mwisho ambayo ikipita, Hatua za Ziada za Kukusanya Deni (ECA) zinaweza kuanzishwa.

**Huduma ya Dharura**: Utunzaji wa mara moja ambao ni muhimu ili kuzuia hatari kubwa kwa afya ya mgonjwa; kulemazwa kwa utendaji wa mwili, na/au utendakazi usio wa kawaida wa viungo au sehemu zozote za mwili.
**Hatua za Ziada za Kukusanya Deni (ECA)** ni orodha ya hatua za kukusanya deni, kama inavyofafanuliwa na Idara ya Hazina, Huduma ya Mapato ya Ndani(IRS) ambayo DCH inaweza tu kuchukua dhidi ya mtu ili kupata malipo ya utunzaji baada ya juhudi za kutosha za kuamua ikiwa mtu huyo anastahiki kupokea msaada wa kifedha. Hatua za ECA dhidi ya mgonjwa zinajumuisha kupata malipo ya utunzaji kutoka kwa mtu mwingine yeyote ambaye amekubali au anahitajika kukubali kuwajibikia malipo ya hospitali ya mtu binafsi kwa huduma hizo (anayejulikana pia kama mdhamini). Hatua za ECA zinajumuisha yafuatayo, lakini sio tu:

a. Katika hali fulani, kuuza deni la mgonjwa kwa mhusika mwingine;

Kutoa ripoti mbaya kuhusu mtu huyo kwa mawakala wa utoaji wa taarifa za mikopo au kampuni za mikopo;

b. Kuahirisha, kukana, au kuitisha malipo kabla ya kutoa huduma muhimu(lakini isiyo ya dharura) ya kimatibabu kwa sababu ya kutolipa kwa bili moja au zaidi za huduma zilizotolewa hapo awali ambazo ziko chini ya FAP ya DCH (inayojulikana kwa ujumla kama"Huduma Iliyoahirishwa");

c. Hatua zinazohitaji mchakato wa kisheria au wa mahakama, pamoja na kuanza hatua ya kiraia dhidi ya mtu binafsi na kuweka dai la kumiliki juu ya mali ya mtu huyo (ingawa kuna hali za kipekee kama vile kuwasilisha ushahidi wa madai ya kufilisika na madai ya hospitali ya kupokea malipo kutoka kwa mhusika wa tatu kwa maamuzi/malipo ya majeraha ya kibinafsi); kuchukua mshahara wa mtu binafsi; kudhibiti au kuchukua akaunti ya benki ya mtu au mali yoyote ya kibinafsi; kumweka mtu chini ya masharti ya kukamatwa; na kusababisha kukamatwa kwa mtu binafsi.

Hatua ya kuweka akaunti ya mgonjwa chini ya udhibiti wa wakala la kukusanya deni sio ECA.

**Watoa Huduma wa Nje**: Kampuni zilizopewa kazi ya kuwa mawakala wa kutoa bili na kukusanya deni.
**Ukubwa wa Familia:** Utajumuisha mgonjwa, mwanandoa wa mgonjwa, bila kujali ikiwa mwanandoa anaishi nyumbani na watoto wote wa mgonwa, aliowazaa au alioasili, chini ya miaka kumi na minane wanaoishi nyumbani.  Ikiwa mgonjwa yuko chini ya miaka kumi na minane, “familia” itajumuisha mgonjwa, wazazi halisi au wa kuasili (bila kujali ikiwa wanaishi nyumbani.

**Kiwango cha Umaskini cha Shirikisho (FPL):**
Kipimo kinachotolewa kila mwaka na Idara ya Afya na Huduma za Binadamu kulingana na mapato ya kila mwaka na ukubwa wa familia ili kuashiria kiwango cha umaskini.
**Msaada wa Kifedha**: Huduma za afya zinazotolewa ambazo hazitarajiwi kusababisha mapato ya kifedha; huduma muhimu za kimatibabu zinazotolewa bila kutoa malipo yanayotarajiwa kwa watu wanaokidhi vigezo vilivyowekwa.
**Fomu ya Maombi ya Msaada wa Kifedha (FAA au Ombi)** inamaanisha hati ambayo lazima ikamilishwe na mgonjwa/mdhamini na kuambatishwa na uthibitisho wa makazi (makazi yanahitajika tu kwa ajili ya Mpango wa HCAP) na mapato, ili kumpa mgonjwa ustahiki wa msaada wa kifedha chini ya Mpango wa Msaada au Mpango wa HCAP.
**Mapato ya Jumla**: Mapato ya jumla kabla ya mapunguzo yoyote kufanywa.
**Mpango wa Uhakikisho wa Huduma za Hospitali** (**HCAP**): Mpango wa Jimbo na Shirikisho unaosimamiwa na Idara ya Medicaid ya Ohio ambayo hutoa fedha kwa hospitali ambazo zina kiasi kikubwa zaidi cha gharama za huduma ambazo hazijalipwa za wakazi wa Ohio wasiojiweza na wasio na bima. HCAP inawapa watu wa Ohio, walio na mapato ya familia yaliyolingana au yaliyo chini ya 100% ya Miongozo ya sasa ya Umaskini ya Shirikisho na wasiostahiki kwa Medicaid ya Ohio, usaidizi wa kulipa bili za hospitali ambazo hazijalipwa.
**Mapato**: Inajumuisha mapato, fidia kwa wasio na ajira, fidia ya wafanyakazi, Usalama wa Jamii, mapato ya ziada ya usalama, misaada ya umma, malipo ya wanajeshi waliostaafu, mafao kwa jamaa za mfanyakazi aliyefariki, mapato ya pensheni au kustaafu, riba, magawio, kodi, mirabaha, mapato kutoka kwa mali, amana, misaada ya kulipia elimu, masurufu, fedha za utunzaji wa watoto, msaada kutoka nje ya familia, na mapato mengine yoyote.  Mafao yasiyo ya pesa taslimu (kama vile vocha za chakula na ruzuku za kulipia makazi) hayajumuishwi.  Mapato huhesabiwa kabla ya mapunguzo yoyote na hayajumuishi faida au hasara katika mali ambayo unamiliki.  Inaweza kujumuisha mapato mengine ambayo hayajafanyiwa kazi ambayo ni pesa za jumla zinazohesabika zilizopokelewa kutoka kwa vyanzo vingine kando na ajira.
**Huduma ya Kimatibabu Inayohitajika**: Huduma za afya au vifaa vinavyotumiwa kwa mgonjwa, anayelazwa na wa nje, ili kutambua ugonjwa, kupunguza, kurekebisha, kuponya, au kuzuia kuanza au kuzorota kwa hali ambazo zinahatarisha maisha, kusababisha kuteseka au maumivu, kusababisha kulemazwa kwa utendakazi wa mwili, kutishia kusababisha au kuzorotesha ulemavu, au kusababisha ugonjwa au udhaifu kwa jumla.
**Kipindi cha Arifa** inamaanisha kipindi cha siku 120 baada ya tarehe ya kwanza ya taarifa ya bili baada ya kuondoka hospitalini, ya matibabu muhimu au matibabu ya dharura yanayohusika.
**Malipo kwa Wakati Mwafaka** ni kulipa dhima ya kifedha inayotarajiwa kabla ya huduma kutolewa au wakati inatolewa.
**Huduma Zinazostahili**

Huduma zinazostahiki chini ya sera hii ya usaidizi wa kifedha ni pamoja na:

- Huduma za matibabu ya kiwewe na ya dharura zinazotolewa katika hali ya dharura.
- Huduma inayotolewa kwa ajili ya hali ambayo itasababisha kuzorota kwa hali ya afya ya mgonjwa isipotibiwa mara moja.
- Huduma za lazima zinazotolewa katika dharura ya matibabu katika chumba kisichotayarishwa kwa ajili ya huduma za dharura.
- Huduma nyingine muhimu za kimatibabu zilizoratibiwa na kuidhinishwa kwa hiari ya DCH.

Huduma zisizostahiki chini ya sera hii ya usaidizi wa kifedha ni pamoja na Ada ya Tabibu, Copays, na huduma fulani za upasuaji za hiari, kama vile upasuaji wa kujirembesha huenda hazishughulikiwi. Ada za kutia unusukaputi, ada ya tafsiri ya Radiolojia zimo kando na malipo ya hospitali na huenda zisistahiki kwa mapunguzo. Orodha ya watoa huduma ambao HAWAKO CHINI YA FAP hii imewekwa kando na sera hii. Umma unaweza kuipata wakati wowote bila malipo katika wavuti ya DCH.

**MAAGIZO:**

**<u>Vigezo vya Ustahiki</u>**

Wagonjwa wowote wanaopokea au wanaonuia kupokea huduma ya dharura au Huduma nyingine Inayohitajika ya Kimatibabu katika Hospitali ya Watoto ya Dayton wanaweza kuomba msaada wa kifedha; hata hivyo, vigezo vinavyotumika kutathmini ustahiki vinaweza kutofautiana kulingana na mahali mgonjwa anapoishi katika tukio ambalo mgonjwa anatafuta huduma isiyo ya dharura.

Wakazi wa Ohio wanaoomba msaada wa kifedha lazima pia waombe Ohio MedicaiD (Healthy Start and Healthy Families) na Mpango wa Uhakikisho wa Huduma ya Hospitali ya Ohio (HCAP). Wakazi wa Ohio wasiohitajika kulipa kodi ya Usalama wa Jamii na Medicare lazima wawasilishe fomu iliyokamilishwa ya 4029 "Ombi la Kusamehewa Kutoa Kodi ya Usalama wa Jamii na Medicare na Msamaha wa Ada ya Mpango wa Mafao" pamoja na maombi yao ya usaidizi wa kifedha ili kuondoa hitaji hili. Wazazi ambao ni wakazi wa Ohio lakini hawastahiki kwa mipango hii na wagonjwa ambao sio wakazi wa Ohio wanaopokea huduma za matibabu ya dharura huko DCH wanaweza kustahiki kupokea msaada wa kifedha kulingana na Jumla ya Mapato ya Jumla na Ukubwa wa Familia kama ifuatavyo:

- Mapato ya Familia ni kiasi sawa na, au yamo chini ya 100% ya Kiwango cha Umaskini cha Shirikisho (FPL) yataondolewa kwa 100% ya kiasi anachodaiwa mgonjwa.
- Mapato ya Familia yamo kati ya 101% na 200% ya FPL yataondolewa kwa 80% ya kiasi anachodaiwa mgonjwa.
- Mapato ya Familia yamo kati ya 201% na 300% ya FPL yataondolewa 60% ya kiasi anachodaiwa mgonjwa.
- Mapato ya Familia yamo kati ya 301% na 400% ya FPL yataondolewa kwa 15% ya kiasi anachodaiwa mgonjwa.
- Wagonjwa wasio na bima walio na mapato ya familia yaliyo zaidi ya 400% ya Kiwango cha Umaskini cha Shirikisho wanaweza kustahiki kupata punguzo la 15%.
- Msaada wa Kifedha kwa COVID-19: Kwa huduma za matibabu zilizotolewa kuanzia kipindi cha Aprili 2020 hadi Juni 2021, Dayton Children huenda ikatoa ustahiki kwa wagonjwa ili wapate punguzo la ziada la COVID-19 la msaada wa kifedha kwenye masalio ambayo hayajalipwa na mgonjwa. Ili kustahiki punguzo hili la bei, mgonjwa/familia lazima itume ombi la msaada wa kifedha kupitia mchakato wa kawaida kama ilivyoainishwa katika sera hii. Hatua ya kukamilika kwa mchakato huu wa maombi itatoa ustahiki kwa mgonjwa/familia, wakati huo, kwa punguzo la bei kwenye masalio ambayo hayajalipwa. Punguzo hili la bei litaanza kutumika kwa hiari ya Hospitali ya Watoto ya Dayton kwa muda unaohusiana na athari ya COVID-19 kwa jamii ya eneo la Dayton.

Taarifa ya Hali ya Kifedha, ombi la Msaada wa Kifedha wa DCH hutumika kuweka rekodi ya hali ya kifedha ya jumla ya mtu binafsi. Msaada wa Kifedha utatolewa tu baada ya bima inayotumika na mipango ya msaada wa serikali imekamilisha ripoti za Mikopo, inaweza kutumika, inapofaa, kuthibitisha hali ya fedha ya mtu binafsi. DCH itaamua ikiwa mgonjwa anastahiki kupokea msaada wa kifedha chini ya sera hii kulingana na jumla ya mapato na ukubwa wa familia kama ifuatavyo katika sehemu ya Asilimia ya Mapunguzo.
Wakati wa kuamua ustahiki wa mgonjwa, Hospitali ya Watoto ya Dayton haizingatii rangi, jinsia, umri, mwelekeo wa kijinsia, ushirika wa kidini, na hali ya kijamii au ya uhamiaji.
Idara ya Uhasibu ya Wagonjwa wa Hospitali ya Watoto ya Dayton itakuwa na mamlaka ya juu zaidi katika kuamua kustahiki kwa msaada wa kifedha chini ya sera hii.

Kwa huduma zilizo na mapunguzo ya chini ya 100% ya Usaidizi, hakuna wagonjwa waliobainika kuwa wanastahiki kupata FAP ambao watatozwa pesa zaidi kwa huduma za dharura au za matibabu yanayohitajika kando na Bili Inayolipishwa kwa Ujumla (AGB) kwa utunzaji au matibabu ya dharura au yanayohitajika.  AGB ni viwango ambavyo hutozwa kijumla kwa huduma za dharura au huduma nyingine za matibabu yanayohitajika kwa watu ambao wana bima za kulipia huduma hizo. Ili kukokotoa AGB, DCH hutumia mbinu ya "kuangalia kumbukumbu".  Katika mbinu hii, DCH hutumia data kulingana na madai yaliyotumwa kwa Medicare, ada za huduma za matibabu za Medicaid, na watoa bima za afya za kibinafsi kwa ajili ya huduma za dharura na za matibabu muhimu kwa zaidi ya miezi 12 iliyopita hivi karibuni, na kuigawanya kwa jumla ya gharama zinazohusiana na madai hayo, ili kubaini asilimia ya malipo ya jumla yanayoruhusiwa na bima hizi.  Hii inaitwa Asilimia ya AGB.  Viasi vinavyohusika vya madai haya vinavyolipwa na watu walio na bima kwa njia ya malipo ya ushirikiano, bima ya pamoja au mapunguzo hujumuishwa katika hesabu ya Asilimia ya AGB. Kisha Asilimia ya AGB huzidishwa na jumla ya gharama za dharura au/na za matibabu muhimu ili kubaini kiwango cha AGB. DCH huhesabu tena Asilimia ya AGB kila mwaka na kusasisha Sera hii kila mwaka ili kuonyesha mabadiliko hayo.  Hivi sasa, DCH hutumia Asilimia zifuatazo za AGB kama ilivyobainishwa hapo juu kwa kiwango cha 52%.

**Mbinu ya Kutuma Ombi la Msaada wa Kifedha**

Maamuzi ya Usaidizi wa Kifedha yatawahitaji wagonjwa kuwasilisha ombi lililokamilishwa la usaidizi wa kifedha (pamoja na hati yoyote ambayo inahitajika) na huenda yakahitaji miadi au majadiliano na mawakili wa kifedha wa hospitali.  Hospitali ya Watoto ya Dayton ina haki ya kuomba nakala za malipo, W-2 na Malipo ya Kodi za Mapato.

Maombi ya Msaada wa Kifedha yanapatikana kwa kuwasiliana na idara ya Akaunti za Wagonjwa kupitia simu kwa (937) 641-5727. Ombi linapatikana kwa ajili ya kupakua kutoka tovuti ya Hospitali ya Watoto ya Dayton. http://www.childrensdayton.org/cms/our_services/index.html
Maombi ya Msaada wa Kifedha yataorodheshwa nyuma ya taarifa ya mgonjwa madhamini.  Wawakilishi wanapatikana ili kuzisaidia familia kwa mchakato wa ombi.  Nakala za karatasi zinapatikana bila malipo kwa mgonjwa anapoziomba.

*Maombi yaliyojazwa yanaweza kurejeshwa kwa njia zifuatazo:*

*Tuma barua kwa: Hospitali ya Watoto ya Dayton*
*Wakili wa Kifedha wa Familia au Mgonjwa*
*Department 1A*
*One Children's Plaza*
*Dayton, Ohio 45404-1815*

*Tuma faksi kwa: 937-641-6601*
*Aione: Wakili wa Kifedha*

*Tuma barua pepe kwa:* FinancialAdvocates@childrensdayton.org

Ombi ambalo halijakamilika likiwasilishwa, barua itatolewa kwa mdhamini ikiomba maelezo zaidi yanayohitajika kukamilisha ombi. Maelezo sahihi ya mawasiliano yatajumuishwa, ikiwa mdhamini ana maswali kuhusu ombi lake.
Mdhamini atatoa anwani ya sasa ya posta katika wakati wa kupokea huduma au wakati atakapohama.

**Uidhinishaji/Ukataaji wa Msaada wa Kifedha**

Hospitali ya Watoto ya Dayton itamwarifu mwombaji ndani ya siku 30 baada ya kupokea ombi lililokamilishwa kuhusu kukubaliwa au kukataliwa kwa ombi la usaidizi wa kifedha.
Baada ya kukubaliwa kwa ombi lililokamilishwa la usaidizi wa kifedha, usaidizi wa kifedha utatolewa ndani ya siku 90 kuanzia tarehe ya uamuzi wa ustahiki, isipokuwa kama ndani ya muda huo wa siku 90, mapato au hali ya bima ya familia ya mtu huyo itabadilika kwa kiasi kwamba mtu huyo hastahiki tena kupata msaada wa kifedha. Hospitali ya Watoto ya Dayton ina haki ya kuwaomba watu hao kudhibitisha tena hali zao ya mapato kabla ya kufanya mapunguzo kwa akaunti za wagonjwa.
Maamuzi kuhusu Usaidizi wa Kifedha huhifadhiwa katika mfumo wa malipo. Kustahiki kwa mgonjwa kutaendelea hadi mwishoni mwa mwezi ambao muda wa kustahiki utamalizika. Katika hali ambapo malipo ya hapo awali yamelipwa, hakuna kiasi kitakachotolewa isipokuwa, ikipitishwa na Mpango wa Uhakikisho wa Huduma ya Hospitali.

**Kutolipa Huduma za Matibabu**

Mdhamini huwajibika kulipa masalio yanayodaiwa na Hospitali ya Watoto ya Dayton. DCH itafanya kila jaribio la kukusanya deni hilo na itafanya juhudi za kutosha za kuamua ikiwa mtu anastahiki kupata Usaidizi wa kifedha. Juhudi za kukusanya deni ni pamoja na kutuma taarifa za mdhamini, kupiga simu na kutumia mhusika wa nje ile kusaidia katika kukusanya deni. Hospitali ya Watoto ya Dayton haitachukua hatua zozote za ziada za kukusanya deni kwa angalau siku 120 (siku mia moja na ishirini) kuanzia tarehe ya taarifa ya kwanza ya mdhamini iliyotumwa na hospitali. Mpango wa malipo (usiozidi muda wa miezi sita) unaweza kukubaliwa na Idara ya Uhasibu ya Wagonjwa. Hospitali ya Watoto ya Dayton inaweza kutumia huduma za mchuuzi wa nje kusaidia kukusanya madeni.

**Upatikanaji wa Sera ya Msaada wa Kifedha na Ombi la Msaada wa Kifedha**

Jitihada zinazofaa ambazo DCH itaweka ni pamoja na zifuatazo:

- Nakala za karatasi zinapatikana bila malipo kwa mgonjwa au mtu anayehusika anapoziomba.
- Nakala za karatasi zinatolewa wakati wa usajili katika maeneo yoyote ya uandikishaji au usajili kwenye kampasi kuu ya Hospitali ya Watoto ya Dayton (ikiwa ni pamoja na Idara ya Dharura) na maeneo ya nje.
- Barua na Maombi ya Usaidizi wa kifedha yanatumwa kwenda kwa waginjwa na/au wazazi ikiwa wataomba.
- Taarifa zote za bili hujumuisha Maombi ya Usaidizi wa Kifedha nyuma ya taarifa hiyo vile vile taarifa za mawasiliano kwa ajili ya idara ambayo inaweza kutoa usaidizi kuhusu maombi.
- Tovuti ya DCH: Maombi yanapatikana kwa ajili ya kupakua kutoka kutoka katika tovuti ya Hospitali ya Watoto ya Dayton. http://www.childrensdayton.org/cms/our_services/index.html
- Muhtasari sahili wa hati hii unapatikana mtandaoni kwenye tovuti ya Hospitali ya Watoto ya Dayton, na unapatikana ikiwa utaombwa na bila malipo katika Idara ya Dharura na maeneo ya Udahili/Usajili.

Arifa na Taarifa Zinazotolewa kwa Wagonjwa wa Hospitalini:

- Bango lililowekwa katika eneo lolote la udahili au usajili katika kampasi kuu ya Hospitali ya Watoto ya Dayton (ikiwa ni pamoja na Idara ya Dharura) na maeneo ya nje ili kuwashauri wagonjwa au mtu anayehusika kuhusu upatikanaji wa usaidizi wa kifedha.
- Washauri wa Masuala ya Fedha wa Hospitali ya Watoto ya Dayton huwatembelea wagonjwa kwa ajili ya usaidizi wa kifedha kwenye vyumba vyao au kliniki.

Mdhamini au mtu anayehusika anashindwa kulipa sehemu yake ya kiasi ambacho anatakiwa kulipa anaweza kuelekezwa kwa wakala kwa ajili ya makusanyo. Mdhamini atapata taarifa nne kabla ya akaunti kutolewa kwa wakala wa kukusanya deni na angalau kupigiwa simu mara mbili.

**Malipo ya Haraka** – Hospitali ya Watoto ya Dayton pia inaweza kutoa punguzo kwa malipo ya huduma ya matibabu ikiwa yatalipwa haraka na kwa wakati.

**Hati Zilizotafsiriwa:**

- Sera ya Usaidizi wa Kifedha, Maombi ya Usaidizi wa Kifedha, na Muhtasari Sahili wa Lugha wa FAP unatolewa katika Kiingereza, Kihispania, Kirusi, Kinyarwanda na Kiswahili. Pia, Wawakilishi wa Huduma kwa Mteja Wanaozungumza Kihispania wanapatikana.

Taarifa za Mawasiliano:

| Washauri | Mahali | Simu |
|---|---|---|
| Hospitali ya Watoto ya Dayton<br>Washauri wa Masuala ya Fedha | Nyenzo kutoka Kwingineko<br>One Children's Plaza<br>8:00am – 5:30pm M-F | 937-641-5727<br>937-641-6601<br>financialadvocates@childrensdayton.org |
| Hospitali ya Watoto ya Dayton<br>Huduma kwa Wateja | Idara ya Akaunti za Mgonjwa<br>Kupiga Simu Pekee | 937-641-3555 |